# Mambo Matano ya kufanya ikiwa mmoja wa mpendwa wako amezuiliwa na ICE au Walinda doria Mipakani

Ilisasishwa mwisho Desemba 19,2025

Mnamo 2025,Marekani imekuwa na ongezeko kubwa la utekelezaji wa ICE na uvamizi wa mahali pa kazi, mahakama za uhamiaji, na maeneo ya umma kama vile barabarani. Ikiwa mpendwa wako amezuiliwa na ICE, au wakara mwingine wa ulinzi wa uhamiaji, hivi ni jinsi ya kuwapata, pata ushauri wa kisheria,andaa hati muhimu, na wape mkono wakati wanapohitaji usaidizi. Hatua hizi zita kupahatua tano muhimu kukusaidia kutatua mchakato huu mgumu:

## 1. Jinsi ya kumpata mpendwa wako


**Hatua ya 1:**Kusanya na sajili mambo muhimu kuhusu kuzuiliwa kwao:

- Tarehe, wakati na mahali pa kukamatwa kwake
- Taja habari tambulizi kuhusu Ofisa aliyemkamata, ikiwemo jina la wakala na numbari ya leseni ya gari(panapowezekana)
- Yaliyosemwa wakati wa kukutana na jinsi Ofisa alikuwa amevaa(kama utambulizi wake haueleweki)
- Muhimu:Kama unashuku mpendwa wako alinyakuliwa na watu wanoa jitambulisha kama waweka usalama, pigia polisi haraka kuripoti uwezekano wa kunyakuliwa.

**Hatua ya 2:** Tafiti katika tovuti ya [ICE Online Detainee Locator System (ODLS).](#)

Unahitajika aidha:

- Majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, na nchi ya kuzaliwa **AU**
- Numbari ya kusajiliwa kama mgeni(A#): Hii numbari ya kipekee ina herufi 9 inayopewa na mamlaka ya uhamiaji unayoweza kuipata kwenye hati rasmi za USCIS, au mahakama ya uhamiaji, au cheti cha kazi. Kama hii ndio mara yako ya kwanza kuhusika na jambo kama hili,utapata numbari mpya A#.
- Elewa*: Mtandao uanweza kosa kuonyesha matokeo ya waliokamatwa kwa muda wa masaa 48 ya kwanza*
- Dokezo muhimu:
    - Jaribu mpangilio tafauti wa majina na chunga makosa ya uchapishaji, hasa kwa majina nyenye herufi za pekee au majina ya mwishi yanayofanana.Km: García Vasquez vs. Garcia-Vazques
    - Jaribu mapngilio tafauti wa tarehe za kuzaliwa, kama vile kubadilisha nafasi ya mwezi na tarehe
    - ODLS haiwezi kutafuta rekodi za walio na umri chini ya miaka 18. Kwa usaidizi kuwapata walio na umri wa chini, familia wanaweza kupigia Ofisi ya kuwapa makao wakimbizi huduma ya kitaifa numbari 1-800-203-7001. Senta hufungua masaa 24 kila siku ya Juma.



# Mambo Matano ya kufanya ikiwa mmoja wa mpendwa wako amezuiliwa na ICE au Walinda doria Mipakani

Ilisasishwa mwisho Desemba 19,2025

**Hatua ya 3:** Ikiwa masafa ya eneo tambulizi ya ICE haitoi rekodi za mpendwa wako, unaweza pia kupigia IC ERO ofisi za nje na maeneo mengine yanayo kuwa na uwezekano wa kuzuia watu. Elewa kuw ICE huwazuiliwa watu kwenye maeneo tofauti tofauti ikiwemo korokoro za ICE, jera za Serikali kuu,na jera za mtaa.
Elewa: *Ni kawaida sana ICE kuhamisha watu kwenye vituo tofauti vya vizuizi nchini kote, bila notisi au maelezo.*

| Wakala | Habari za mawasiliano(mitandao) | Ya kuzingatiwa | QR Code |
|---|---|---|---|
| **ICE** | • Ofisi za nje za Utekelezaji na uondoaji wa ICE<br>• Vituo vya kizuizini vya ICE | Tafuta kituo cha kizuizi cha ICE au ofisi ya mtaa iliyo karibu na maeneo alipozuiliwa. | |
| **Ofisi ya magereza** | Masafa tambulizi ya wakamatwa ya Ofisi ya magereza | Jera za Serikali Kuu zilizotumika kuwazuilia watu waliovoju hatia za za Serikali kuu, kwa sasa zianatumika kuwazuilia watu wanazo kesi za kuondolewa nchini. | |
| **Ubalozi** | Maelezo ya mawasiliano na Balozi za kigeni & ubalozi | Wahamiaji waliozuiliwa wana haki za msaada wa kibalozi. Ingawa vile, kama mpendwa wako anaomba hifadhi na anaogopa serikali yake, kufikia ubalozi kunaweza kuathiri uhifadhi wao. | |

## 2. <u>kusanya hati muhimu</u>

Andaa na uweke nakala za hati unazohitaji kutetea kesi yako. Kuwa na hati hizi tiyari kutasaidia wakili wako kuandaa kesi yenye msingi dhabiti.
Hizi ni pamoja na:

- Vitambulisho(pasipoti,Kitambulisho cha Jimbo)
- Hati za uhamiaji(visa, notisi za mialiko)
- Vyeti vya kuzaliwa na ndoa

- Rekodi za matibabu
- Hati za kisheria za mbelini au za mahakama

### 3. <u>Kutafuta uwakilishaji wa kisheria & kutambulisha tarehe ya kesi yao katika Mahakama ya uhamiaji</u>

Unaweza kutazama hali na tarehe ya kusikizwa kesi kwa mpendwa wako katika mtandao wa EOIR Case Status Portal or au kupiga simu ya otomatiki ya EOIR (1-800-898-7180). Utahitaji numba A na uraia wa mpendwa wako.

Ufadhili wa kisheria ni muhimu. Unaweza kuwasiliana na wakili binafsi wa uhamiaji au mhudumu wa kisheria kutoka shirika la uhamiaji lisilo la faida ili kuelewa chaguzi zoa katika kuondolew au ustahiki wa dhamana na kuendele kwa mchakato. Unaweza kutafuta mawakili binafsi wa uhamiaji katika maeneo yako kupitia orodah ya mawakili wa Chama cha mawakili wa uhamiaji wa marekani 'American Immigration Lawyers Association' au Mradi wa watetezi wawanaotafuta hifadhi "Asylum Seeker Advocacy Project (ASAP)". Saraka ya kitaifa ya huduma ya kisheria ya uhamiaji "The National Immigration Legal Service Directory" iko n a orodha ya watoa huduma za kisheria wasio na faida katika eneo lako. Kwa sababu ya uhitaji uliongezeka, kupata usaidizi kutoka kwa mwakilishi kwa haraka kunaweza kuleta changamoto. Unaweza pia kufikia usaidizi wa dharura wa maeneo yako kupitia "Rapid Response Network of Hotlines" kwa msaada wa dharura.

| | |
|---|---|
| **jukwaa la hali ya kesi la EOIR "EOIR Case Status Portal"** | |
| **Saraka ya kitaifa ya huduma ya kisheria ya** | |
| **Mtandao wa harakati za dharura "Rapid Response Network of Hotlines"** | |
| **Chama cha wanasheria wa uhamiaji wa Marekani** | |
| **Orodha ya mawakili binafsi ya ASAP** | |

### 4. <u>Kaa chonjo na toa msaada</u>

Mara tu mpendwa wako atafika kituo cha kizuizini , wanaweza kuuliza nafasi ndogo kupiga simu ya bure kwa mmoja wanaochagua. Tia maanani wanaweza tu kupiga simu nambari walizoweka kwa Kichwa tu. <u>Kuwa tayari kupoke simu zao.</u>

Baadaye ,walio na fedha katika akaunti ya commissary wanaweza kupiga simu kutoka kwa vyumba vyao. Kama kuna dharura ya kifamilia na mpendwa wako hana fedha za kutosha, anaweza kuuliza nafasi kutoka kwa msimamizi wa nyumba au mfanyakazi wa ICE kupiga simu za bure.

*Tafadhari elewa kuwa simu nyingi zinaweza kupelelezwa na kurekodiwa na ICE,ila to simu kwa wakili au ubalozi wao, inayochukuliwa ya faragha.*

Mara tu unapompata mpendwa wako, wasiliana na kituo cha kizuizi kuelewa mengi kuhusu chaguzi za mawasilaino. Vituo kadhaa huruhusu wageni kutembea,hali vingine huruhusu tu simu za video. <u>Kama huna hali ya uhamiaji pia, **usiende** kutemebea vizuizi vya uhamiaji</u>.

# Mambo Matano ya kufanya ikiwa mmoja wa mpendwa wako amezuiliwa na ICE au Walinda doria Mipakani

Ilisasishwa mwisho Desemba 19,2025

Bidhaa kama vile nguo au chakula haviruhusiwi,vituo vya vizuizi huvitoa . Walakini, bidhaa kama vile stakabadhi rasmi, vitabu na barua vinaweza kuruhusiwa kulingana na sera za kituo. Kama ungependa kutuma pesa kwamatumizi banafsi au chakula cha ziada, uliza kituo cha kizuizi jinsi vile unaweza kuchangia akaunti ya commissary ya mpendwa wako.

*Akaunti ya mommisary huhifadhi pesa zozote walizokuwa nazo wakati wa kuzuiwa na fedha zote wakatazopokea wakiwa ndani. Wanaweza kutumia pesa hizi kunua stamp, kupiga simu, kunua vitafuno au bidhaa zingine. Kama mpendwa wako amehamishwa, ICE lazima ibebe mabaki kwa kituo kingine. Mabaki yoyote lazima yarudishwe wakati wa kuachiliwa au kuondolewa Marekani.*

### 5. kinachtendeka kwa kesi ya mpendwa wako baada ya kitiwa kizuizini?

Mpendwa wako anaweza kuwa na haki ya kusikizwa mbele ya hakimu wa uhamiaji. Baadhi ya watu hawastahiki kusikizwa, kwa mfano kwa sababu za makataa ya kuondolewa yanayoendelea(kama walikuwa mbelenin wametolewa ilani ya kuondolewa lakinin hawakutoka), kama wana mchakato wa kusikizwa kwa dharura kuondolewa kwao na hawakukutaja hofu kurejea nchi yao ya asili, au kama walikuwa wameondolewa lakini wakarudi tena Marekanin bila idhini. Kutegemea hali ya kesi , mpendwa wako anaweza kupata nafasi ya kuachiliwa kwa dhamana au kuachiliwa huru anapozidi kungojea wakati wa kusikizwa kesi yao

Kama mpendwa wako ana maswali kuhusu kesi yao au chaguzi za kisheria, wanaweza pigia wakili aliyekatika orodha ya ICE ya watoa huduma za bure tmia simu faragha kwenye chumba chako cha kizuizi. *Huduma hizi zinatakiwa kwa juu sana, kwa hivyo endele kujaribu kupiga unapopata jibu laini zinatumika*. Wanaweza pia kupigia Chama cha wanasheria wa marekani(ABA) nambari 215# ya habari za mwelekeo wa kisheria huduma faragha kutoka ndani ya chumba cha ICE.

### Rasilmali za ziada

| | |
|---|---|
| **Mradi wa kitaifa wa uhamiaji- Mwanajamii wa jamii yangu alikamatwa na ICE, je natakiwa nifanye nii? ( inapatikana kwa lugha hizi English, Spanish, Haitian Creole)** | |
| **Elewa haki zako:Mambo Matano wazazi waliotiwa kizuizi na ICE wanayotakiwa kuelewa(yanapatikana kwa lugha hizi English, Spanish, Haitian Creole)** | |
| **ImportaMi ina** makala **muhimu inayo habari kuhusu unayotakiwa kufanya kama umepata habari ya makataa yakuondolewa nchini** | |
| **Kama unahitaji msaada zaidi kutafuta numba A, rejelea** makala **ya Importa Mi** | |